

Mungu hu fatilia neno lake.  
Anza kila siku na mstari  
mfukoni mwako na tembeya  
naye. Mistari ya juma hili  
inahusu "Majaribu"

Ee Mungu, uniumbie  
moyo safi, Uifanye upya  
roho iliyotulia ndani  
yangu  
**Zaburi 51:10**

Msifungiwe nira pamoja na  
wasioamini, kwa jinsi isivyo  
sawasawa; kwa maana pana  
urafiki gani kati ya haki na  
uasi? **2 Wakorintho 6:14**

Na kwa kuwa mwenyewe  
aliteswa alipojaribiwa,  
aweza kuwasaidia wao  
wanaojaribiwa.  
**Waebania 2:18**

Kesheni mwombe, msije  
mkaingia majaribuni,  
roho i radhi ila mwili ni  
dhaifu.  
**Marko 14: 38**

Moyoni mwangu  
nimeliweka neno lako,  
Nisije nikakutenda  
dhambi  
**Zaburi 119: 11**

Kwa maana mshahara wa  
dhambi ni mauti; bali karama  
ya Mungu ni uzima wa milele  
katika Kristo Yesu Bwana  
wetu. **Warumi 6: 23**

Mungu hu fatilia neno lake.  
Anza kila siku na mstari  
mfukoni mwako na tembeya  
naye. Mistari ya juma hili  
inahusu "Baba yetu"

Baba wa yatima na  
mwamuzi wa wajane,  
Mungu katika kao lake  
takatifu  
**Zaburi 68:5**

Mwanangu, yasikilize  
mafundisho ya baba  
yako, Wala usiiache  
sheria ya mama yako,  
**Methali 1:8**

Sitawaacha ninyi  
yatima; naja kwenu.  
**Yohana 14: 18**

Naye ataigeuza miyo ya baba  
iwaelekee watoto wao, na  
miyo ya watoto iwaelekee  
baba zao, ili nisije nikaipiga  
dunia kwa laana. **Malaki 4:6**

Baba yake mwenye haki  
atashangilia; Naye amzaaye  
mtoto mwenye hekima  
atamfurahia  
**Methali 23:24**

Basi ninyi salini hivi;  
Baba yetu uliye  
mbinguni, Jina lako  
litukuzwe, Ufalme wako  
uje, **Matayo 6:9**

Mungu hu fatilia neno lake.  
Anza kila siku na mstari  
mfukoni mwako na tembeya  
naye. Mistari ya juma hili  
inahusu  
"Kumtumainiya Mungu"

Jina la Bwana ni ngome  
imara; Mwenye haki  
huikimbilia, akawa  
salama. **Methali 18:10**

na kuwafundisha kuyashika  
yote niliyowaamuru ninyi; na  
tazama, mimi nipo pamoja  
nanyi siku zote, hata ukamilifu  
wa dahari. **Matayo 28:20**

Mtumaini Bwana kwa  
moyo wako wote, Wala  
usizitegemee akili zako  
mwenyewe;  
**Methali 3:5**

Nayaweza mambo yote  
katika ye ye anitiaye  
nguvu  
**Wafilipi 4:13**

...Nitaiharibu hekima yao  
wenye hekima, Na akili  
zao wenyewe akili nitazikataa  
**1 Wakorinto 1:19**

...Ni Yeye aendaye katika  
giza, wala hana nuru, naye  
alitumainia jina la Bwana, na  
kumtegemea Mungu wake.  
**Isaya 50: 10**